**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**Tarehe: 12/12/2020**

**KUMB. MIR/SS/FI/2021/0001**

**MZAZI/MLEZI WA …………………………………………..………………….**
……………………………………………………………………..…………….….
…………………………………………………………………………….…….**.**

**YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO**
**KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIRUI KWA MWAKA WA MASOMO 2021.**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika **Shule ya Sekondari MIRUI** kwa mwaka wa masomo **2021**

Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.

**Shule ya Sekondari MIRUI** ipo **Mkoa wa Lindi Wilaya ya LIWALE.** shule ipo umbali wa km 88 kutoka makao makuu ya wilaya ya LIWALE. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** bila ya kukosa.

Pamoja na barua hii, pokea,

(a) Fomu ya kupimwa afya yake. Apimwe kwenye Hospitali ya Serikali, hakikisha anapimwa sio kujaziwa fomu tu, na umwelekeze Mganga matatizo ya afya uliyonayo, kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya daktari.
(b) Fomu ya kuonyesha ndugu wa karibu ikiwa na anuani, namba ya simu na mahali anakoishi pamoja na ahadi ya kutekeleza wajibu. Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunga nasi.

**KARIBU MIRUI SEKONDARI**

…………………………………….

IMANI R. MINTANGA

MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

**A. Sare ya shule:**

**WAVULANA**

- Suruali ya kushona rangi ya dark bluu urefu na upana uwe wa heshima na iwe ya linda mbili na isiwe na "turn up" isibane na iwe ndefu ifunike kiatu
- Shati rangi nyeupe mikono mifupi lisioneshe mwili wa ndani
- Viatu rangi nyeusi vya ngozi na viwe vya kamba, kisigino kiwe kifupi
- Soksi nyeupe
- Mkanda mweusi wa ngozi

**WASICHANA**

- Sketi rangi ya dark bluu iwe ndefu na ya heshima na iwe na malinda ya kawaida (kitambaa kizito)
  N.B; Wanaovaa hijabu washone nusu kanzu kwa wasichana
- Shati rangi nyeupe mikono mifupi lisioneshe mwili kwa ndani (vitambaa vya saatini nyeupe kiwe cha hijabu au shati haviruhusiwi)
- Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi (viatu aina ya bajaji haviruhusiwi)
- Soksi nyeupe na ziwe ndefu
  N.B: Na inasisitizwa kwamba mwanafunzi ni marufuku kuvaa nguo nyingine ndani ya sare ya shule kwa wakati mmoja

**WANAFUNZI WANAOKUJA KUKAA SHULENI(HOSTELI)**

Anatakiwa ashoneshe sketi nyeusi ndefu na awe na fulana nyekundu, nguo zingine tofauti na hizo hataruhusiwa kuzivaa au kuja nazo shuleni

**B. VIFAA VYA MASOMO**

i. Begi ya kuwekea daftari na vifaa vingine ii. daftari kubwa 12 iii. mathematical set (mkebe) iv. kamusi ya kiingereza (dictionary) v. karamu ya risasi vi. Rula futi moja vii. Peni ya bluu/nyeusi viii. Rim moja ya karatasi A4

**C. PIA TUNA NAFASI ZA KUKAA SHULENI(HOSTELI) KWA WASICHANA KWA MZAZI ANAYETAKA ATACHANGIA VITU VIFUATAVYO**

Mahindi kg 70,kunde maharage mbaazi kwa kila kimoja achangie kilo 5 dagaa kg 3 mafuta lita 3 mchele kg 12 chumvi kg 2 vitunguu kg 3 pesa ya kusagia 7000 iwapo ataleta mahindi yasiyosagwa na akatiwe bima ya afya na godoro la futi mbili na nusu kwa sita

N.B: Ili mwanafunzi akae shuleni sharti achangie nusu ya vyakula vinavyohitajika

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

## ANGALIZO KWA MZAZI

i. Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa ni mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.
ii. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni.
iii. Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.
iv. Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.
v. Siku ya kuwatembelea wanafunzi ni Jumamosi na Jumapili tu, muda ni kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi na moja jioni kwa wanafunzi wanaokaa shuleni na mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani tarehe ya mwisho wa mwezi tu.
vi. Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo
vii. Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa mwalimu wa malezi wa shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Asipofanya hivyo shule itashindwa kumuhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yake.
viii. Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake
ix. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA MASOMO MARA MOJA)
x. Viatu aina ya ndala, kito (open shoes),yeboyebo,buti au bajaji ni marufuku kuvaliwa shuleni labda awe na ugonjwa uliothibitishwa na daktari.

**N.B**: Tafadhari mshauri mwanao azingatie/afuate maelekezo yote aliyopewa!
Akipatikana na kosa shule itamchukulia hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**<u>Sheria za shule</u>**

(a) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote
(b) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa
(c) mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k
(d) Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote
(e) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa
(f) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani wakati wa kujisomea.
(g) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake
(h) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, earphones’’ pamoja na redio
(i) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia ofisi ya makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi tu.
(j) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani kwa wanaokaa shuleni.
(k) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani au hospitalini mitaani. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na uongozi wa shule
(l) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.
(m) Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl,nywele za bandia, mapambo kama bangili, heleni, mikufu n.k. havitakiwi kabisa shuleni
(n) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa,Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani (kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizo.
(o) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, bila ya ruhusa ya mwalimu.
(p) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa
(q) Mwanafunzi **haruhusiwi kusuka nywele**, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni, urefu unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana. Haruhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k
(r) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo shuleni
(s) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika katika eneo la mabwenini
(t) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa kwa kusalimia tu.
(u) Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shule ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo
(v) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la kinidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba, shangazi, kaka n.k.

(w) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupigana na mtu yeyote awapo shuleni
(x) Mwanafunzi haruhusiwe kutumia lugha chafu.

(y) Mwanafunzi haruhusiwi kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(z) Mwanafunzi haruhusiwi kuanzisha, kushawishi na kushiriki mgomo.

**Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo kwa muda (suspension) iwapo atakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule:**

**N.B: Mwanafunzi atakayeharibu miundombinu ya shule mzazi/mlezi wake atawajibika kutengeneza au kununua ili kufidia huo uharibifu uliofanywa na mtoto husika.**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

## KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA *KWANZA* KWA MWAKA 2021

**Mimi** ………………………………………………………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari MIRUI. **NIMEKUBALI/NIMEKATAA** nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari MIRUI. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

**Jina la mwanafunzi** ……………………………………..……… **Saini** …….……….…

**Tarehe** ……………………

**Jina la Mzazi/Mlezi** ……………………………………..……… **Saini** ……………..…

**Tarehe** ……………………

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**FOMU NAMBA 1.**

**To the Medical Officer**
……………………………………………………………………….…
……………………………………………………………………….**.**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO …….…………………………………………**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood……………………………………………………………………………………..
2. Stool ……………………………………………………………………………………..
3. T.B. Test ……………………………………………………………………………….
4. Syphilis Test ……………………………………………………………………………..
5. Urine Examination ……………………………………………………………………….
6. Eye Test ………………………………………………………………………………….
7. Chest Test ………………………………………………………………………………...
8. Ears Test ………………………………………………………………………………….
9. Spleen …………………………………………………………………………………….
10. Abdomen …………………………………………………………………………………
11. Pregnancy…………………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

Name of **Medical Officer**: …………………………………………… Signature ………………………
Date: ……………………………………… Official stamp ………………………………

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Mkoa ………………..……………………… Wilaya …………………………………………
2. Tarafa ……………………………………………. Kata …………………………………………
3. Mtaa/Kijiji ……………………………………………
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………..………….Saini………………….
   Tarehe………………………………. Mhuri…………………………… Simu…………………...
5. Michezo anayopendelea

| Na. | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

9. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na. | Aina ya Uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

**NB**: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na cheti chako cha kuzaliwa.

**Jina la Mwanafunzi ……………………………………..Sahihi ………………… Tarehe ……………**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………….
2. Kazi ……………..…………………………………………………………………………...
3. Anuani …………………………………………… Namba ya simu ……………………………….
4. Mkoa ………………………… Wilaya ……………………….. Tarafa ………….……………….
5. Kata ………………………………………Mtaa/Kijiji …………………………………………….

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari MIRUI katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

**Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………………Sahihi …………………Tarehe ………………..**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**

**MKOA: LINDI**
SIMU: 0623966228/0714494848
0624002687/0624445217

SHULE YA SEKONDARI MIRUI
S.L.P 50,
**LIWALE.**